# MKUTANO MKUU
# WA 25 WA WANAHISA
# TAREHE 27.06.2020

UTAKAOENDESHWA KWA NJIA YA KIDIGITALI




Tunasonga mbele

CRDB BANK
Tunakusikiliza

# Mshirika wako katika maendeleo

Fahari Kilimo

Mafanikio kwa jamii

Niamoja
ACCOUNT

Mafanikio kwa wanakikundi

CRDB BANK
Tunakusikiliza



# POPOTE INATIK✓

Kimbiza miamala yako upendavyo.

SimBanking

ATM

POS

WAKALA

WAKALA

INTERNET BANKING

SCAN, LIPA, SEPA

PIGA

*150*03#

PAKUA KWENYE

CRDB BANK

*Tunakusikiliza*

*Mwenyekiti na Wanahisa,*

**YAH: TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA ISHIRINI NA TANO**

Rejea taarifa iliyochapishwa kwenye vyombo vya habari kuhusu kuahirishwa kwa Mkutano Mkuu uliopangwa kufanyika tarehe 16 Mei, 2020.

**TAARIFA inatolewa kwamba MKUTANO MKUU WA ISHIRINI NA TANO wa Wanahisa wa** CRDB BANK PLC utafanyika siku ya Jumamosi, tarehe 27 Juni, 2020 kuanzia saa tatu kamili asubuhi na wanahisa watashiriki kwa njia ya kidijitali.

Benki itafanya Mkutano Mkuu mwaka huu kwa njia ya kidijitali ili kuepuka uwezekano wa maambukizi ya ugonjwa wa Corona kutokana na idadi kubwa ya wanahisa wanaotegemewa kuhudhuria Mkutano Mkuu na kutokuwepo Ukumbi wenye nafasi ya kutosha kwa washiriki wote wakiwa wamekaa na kutimiza taratibu na masharti yanayowataka watu kutokukaribiana na kupeana nafasi ili kujikinga dhidi ya maambukizi. Benki inachukulia kwa umuhimu wa kipekee afya na usalama wa wanahisa na wadau wake wote. Kwa kuwa na dhamana na wajibu kwa jamii, Benki inaunga mkono juhudi za Serikali kupambana na ugonjwa wa Corona kwa kuzingatia taratibu zote za kiafya zinazotakiwa kufuatwa kama vile kuepuka mikusanyiko na kuzingatia watu kutokusongamana kwa kuachiana nafasi.

Benki itawatumia wanahisa wote kupitia simu zao za mkononi utambulisho na maelekezo kuhusu jinsi ya kujiunga na kushiriki Mkutano Mkuu kidijitali. Azimio maalum litapitishwa na wanahisa ili kuruhusu Mkutano Mkuu ufanyike kwa njia ya kidijitali.

Dondoo zifuatazo zitajadiliwa:

1. **Kufungua Mkutano.**
2. **Kuchagua Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Mkutano Mkuu.**
3. **Azimio Maalum kuidhinisha marekebisho kwenye Katiba ya Benki (MEMARTS) kuruhusu Mkutano Mkuu kufanyika kidijitali.**
4. **Kuridhia dondoo.**
5. **Kuthibitisha kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa Ishirini na Nne.**
6. **Kujadili yatokanayo.**
7. **Kupokea Taarifa ya Bodi ya Wakurugenzi na Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa za Mwaka 2019.**
    a) Taarifa ya Bodi ya Wakurugenzi.
    b) Hesabu zilizokaguliwa kwa Mwaka ulioishia tarehe 31 Disemba, 2019.
    c) Azimio la Gawio kwa Mwaka 2019.
8. **Kuidhinisha ada ya Wakurugenzi.**
9. **Kuteua Wakaguzi wa nje wa Hesabu.**

**Taarifa** ya Mkutano Mkuu

**10. Kuchagua wajumbe wawili Huru wa Bodi.**

**11. Kujadili mapendekezo kutoka kwa Wanahisa.**

**12. Mengineyo kwa idhini ya Mwenyekiti.**

**13. Kupanga mahali, ukumbi na tarehe ya Mkutano Mkuu ujao.**

**14. Kufunga Mkutano.**

***MAELEZO:***

1. *Daftari la Wanahisa litafungwa tarehe 26/06/2020 na litafunguliwa tarehe 27/06/2020.*
2. *Mapendekezo yote kutoka kwa wanahisa yatakayojadiliwa katika dondoo namba 12 yatumwe na kumfikia Katibu kabla ya saa 10.00 jioni siku ya Ijumaa tarehe 12 Juni, 2020.*
3. *Taarifa ya Mwaka 2019 na Makabrasha ya Mkutano yatapatikana kwenye tovuti ya Benki (https://www.crdbbank.co.tz) na matawi ya Benki kuanzia siku ya Ijumaa tarehe 12, Juni, 2020.*
4. *Wanahisa wanaombwa kuteua wawakilishi watakaohudhuria mkutano kwa niaba yao . Fomu ya Uwakilishi inapatikana kwenye tovuti ya Benki (https://www.crdbbank.co.tz).*
5. *Fomu za Uwakilishi zilizojazwa zitumwe kwa Katibu kupitia barua pepe shareholders@crdbbank.com au zipelekwe kwenye tawi lolote la Benki ya CRDB, au picha ya fomu ya uwakilishi iliyojazwa itumwe kwenye WhatsApp na.0767757215 na kumfikia Katibu kabla ya saa 10.00 jioni siku ya Jumatatu tarehe 22 Juni , 2020.*
6. *Kutokana na kuahirishwa kwa Mkutano Mkuu wa 25 wa Wanahisa, uliokuwa umepangwa kufanyika tarehe 16 Mei 2020 na kuwa tarehe 27 Juni 2020, tarehe ya ulipaji wa gawio la mwaka 2019 pia imebadilishwa kutoka tarehe 1 Juni 2020 kuwa tarehe 30 Juni 2020 baada ya kuidhinishwa na Mkutano Mkuu wa Wanahisa utakaofanyika tarehe 27 Juni 2020.*

Kwa mawasiliano tumia anuani ifuatayo:

**Katibu**
**CRDB Bank Plc**
**Office Accommodation Scheme- Azikiwe Street, 4th Floor**
**S.L.P. 268**
**DAR-ES-SALAAM.**
**Simu. na. 022 - 2114237, 2117442 - 7**
**Barua Pepe -** shareholders@crdbbank.com

**KWA IDHINI YA BODI**

J. B. Rugambo
**KATIBU**

*20 Mei, 2020*

## FOMU YA UWAKILISHI

## MKUTANO MKUU WA 25 WA WANAHISA

1. Mimi/Sisi ______________________________CDS A/C NO: ___________________
nikiwa/tukiwa wanahisa wa Benki ya CRDB mwenye/wenye haki ya kupiga kura ninamteu /tunamteua:

_______________________________________of ______________________________
aniwakilishe/atuwakilishe kuhudhuria, kuzungumza na kupiga kura kwa niaba yangu/yetu katika Mkutano Mkuu wa Wanahisa wa Benki ya CRDB utakaofanyika tarehe 27 Juni, 2020 na pale utakapoahirishwa.

**MUHIMU**:

a. Kifungu namba 138 cha Sheria ya Makampuni kinampa mamlaka mwanahisa kumteua mtu mwingine kuhudhuria, kupiga kura na kuzungumza kwa niaba yake katika Mkutano Mkuu wa wanahisa. Mwakilishi anayeteuliwa sio lazima awe mwanahisa.

b. Ibara ya 59 ya Katiba ya Benki ya CRDB inaelekeza taarifa za uwakilishi wa mwanahisa kutumwa katika ofisi rasmi/ iliyosajiliwa ya Kampuni katika kipindi kisichopungua saa 72 kabla ya muda uliopangwa kwa ajili ya Mkutano.

2.Nimeweka/tumeweka alama “X” kuonesha ninavyotaka/tunavyotaka kura yangu/yetu ipigwe kwenye maazimio yafuatayo:

| S/N | MAAZIMIO | NDIYO | KUPINGA | KUACHA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Kufanya Mkutano Mkuu wa 25 wa Wanahisa mwaka 2020 kwa njia ya mtandao. **AZIMIO MAALUM** linalohitaji **75%** ya kura | ○ | ○ | ○ |
| 2 | Kupokea Taarifa ya Wakurugenzi. | ○ | ○ | ○ |
| 3 | Kupokea Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa kwa mwaka ulioshia tarehe 31 Desemba, 2019. | ○ | ○ | ○ |
| 4 | Gawio kwa Mwaka 2019 | ○ | ○ | ○ |
| 5 | Kuidhinisha ada ya Wakurugenzi | ○ | ○ | ○ |
| 6 | Kuteua Wakaguzi wa nje wa Hesabu. | ○ | ○ | ○ |
| 7 | Kupanga Mahali, Tarehe na Ukumbi wa Mkutano Mkuu ujao. | ○ | ○ | ○ |

3.Ninamuelekeza/tunamuelekeza mwakilishi/wawakilishi wangu/wetu kupiga kura kama ifuatavyo:

Kuchagua wagombea wawili wafuatao kuwa Wajumbe Huru wa Bodi: (Weka alama "X" kwenye jina la mgombea unaemchagua kuwa Mjumbe wa Bodi )

**UCHAGUZI WA WAJUMBE WAWILI HURU WA BODI**

| S/N | JINA | KURA |
|---|---|---|
| i) | Prof. Neema Munisi Mori | |
| ii) | Bi. Miranda Naiman Mpogolo | |
| iii) | Bi. Hilda Shenyagwa-Noor | |
| iv) | Bw. Damas Damian Mugashe | |

Imetiwa saini Tarehe ______________ Mwezi ______________ Mwaka 2020

Saini ya Mwanahisa ________________Namba ya Simu: ____________________

Barua Pepe: _______________________________________



Mgombea wa nafasi ya
Mjumbe Huru wa Bodi

**Bi. Hilda Shenyagwa-Noor**



Mgombea wa nafasi ya
Mjumbe Huru wa Bodi

**Prof. Neema Munisi Mori**



Mgombea wa nafasi ya
Mjumbe Huru wa Bodi

**Damas Damian Mugashe**



Mgombea wa nafasi ya
Mjumbe Huru wa Bodi

**Bi. Miranda Naiman Mpogolo**

## SUMMARY OF CANDIDATES' CVs

| S/N | Name/Age/ Address<br><br>Jina/Umri/ Anuani | Curent position<br><br>Kazi ya Sasa | Educational Qualification<br><br>Elimu/Taaluma | Work Experience<br><br>Uzoefu |
|---|---|---|---|---|
| 1. | **Name**: **Prof. NEEMA MUNISI MORI**<br><br>**Address:** P. O. Box 35046 Dar es Salaam<br><br>**Age:** 41<br><br>**No. of Shares: 118,084**<br><br>**CDS A/c No. 131043** | **2019 to date**<br><br>Associate Professor<br><br>University of DSM<br><br>**2019 to date**<br><br>Chairperson of Board Credit Committee and<br><br>Board Vice Chairperson, CRDB Bank Plc Board of Directors<br><br>**2017 to date**<br><br>Board Member, CRDB Bank Plc<br><br>Certified Director, IoD UK | **2008 – 2012**<br><br>PhD in International Business majoring in Corporate Governance and Boards of Micro Finance Institutions,<br><br>University of Agder, Norway<br><br>**2002 – 2004**<br><br>Master of Business Administration (MBA) in Finance, University of DSM<br><br>**1999 – 2002**<br><br>Bachelor of Commerce (B.Com) majoring in Finance,<br><br>University of DSM | **2016 – 2019**<br><br>Senior Lecturer, Department of Finance,<br><br>University of DSM<br><br>**2013 – 2015**<br><br>Lecturer, Department of Finance, University of DSM<br><br>**2013 – 2015**<br><br>Post-Doctoral Research Fellow, Norwegian Centre for Microfinance Research<br><br>University of Agder, Norway<br><br>**2005 – 2012**<br><br>Assistant Lecturer, Department of Finance, UDSM |

**Prof. NEEMA MUNISI MORI**



| S/N | Name/Age/ Address<br><br>Jina/Umri/ Anuani | Curent position<br><br>Kazi ya Sasa | Educational Qualification<br><br>Elimu/Taaluma | Work Experience<br><br>Uzoefu |
|---|---|---|---|---|
| 2. | **Name: MIRANDA NAIMAN MPOGOLO**<br><br>Address: P.O. Box 105552 DSM<br><br>Age: 37 | **2009 to date**<br><br>Founder and Managing Director<br><br>Empower Limited<br><br>**2020 to date**<br><br>Board Member - African Women Entrepreneurship Cooperative<br><br>**2018 to date**<br><br>Board Audit Committee - Tanzania Private Sector Foundation<br><br>**2018 to date**<br><br>Advisory Board Member, AIESEC | **2004 – 2005**<br><br>Master of Arts, Theatre & Development Studies (Merit), University of<br><br>Leeds, UK<br><br>**2001 – 2004**<br><br>Bachelor of Arts (Hons) Drama, Applied Theatre and Education<br><br>Central School of Speech and Drama, UK | **2006 – 2008**<br><br>Training Manager - Radar Limited<br><br>**2005 – 2006**<br><br>Recruitment Consultant<br><br>Radar Limited<br><br>**2004 – 2005**<br><br>Applied Theatre Practitioner, West Yorkshire Playhouse |

**MIRANDA NAIMAN MPOGOLO**



| S/N | Name/Age/ Address<br><br>Jina/Umri/ Anuani | Curent position<br><br>Kazi ya Sasa | Educational Qualification<br><br>Elimu/Taaluma | Work Experience<br><br>Uzoefu |
|---|---|---|---|---|
| 3. | **Name: HILDA SHENYAGWA NOOR**<br><br>Address: P.O. Box 42 DSM<br><br>Age: 43 | **2008 to date**<br><br>Senior Underwriter,<br><br>Tanzania Reinsurance Company Limited (TAN-RE) | **2017**<br><br>Member of the Chartered<br><br>Insurance Institute (CII), UK<br><br>**2008 – 2010**<br><br>Master of Business Administration (MBA) Eastern and Southern African Management Institute (ESAMI), DSM<br><br>**2001 - 2003**<br><br>Bachelor of Business Administration (BBA) majoring in Economics and Finance, Institut Supérieur de Gestion (ISG), Paris, France.<br><br>**1998 - 1999**<br><br>French Language and Civilisation Certificate,<br><br>University of Paris IV | **2008**<br><br>Senior Manager – Broker<br><br>AON Tanzania Ltd, Dar es Salaam, Tanzania<br><br>**2003 - 2007**<br><br>Reinsurance Broking Assistant<br><br>Afro - Asian Insurance Services, London, U.K. |

**HILDA SHENYAGWA NOOR**



| S/N | Name/Age/ Address<br><br>Jina/Umri/ Anuani | Curent position<br><br>Kazi ya Sasa | Educational Qualification<br><br>Elimu/Taaluma | Work Experience<br><br>Uzoefu |
|---|---|---|---|---|
| 4. | **Name: DAMAS DAMIAN MUGASHE**<br><br>Address: P. O. Box 1046 DSM<br><br>Age: 51 | **2018 to date**<br><br>Director of Finance and Business Operations - Tanzania Institute of Bankers | **2002 - 2004**<br><br>Master of Business Administration<br><br>ESAMI Business School, Arusha<br><br>**2000**<br><br>Certified Public Accountant - CPA (T)<br><br>**1996 - 1997**<br><br>Post Graduate Diploma in Financial Management -<br><br>Institute of Finance Management (IFM)<br><br>**1993 - 1996**<br><br>Advanced Diploma in Accountancy - IFM | **2011 – 2018**<br><br>Finance Management Specialist, World Bank Projects, Bank of Tanzania<br><br>**2008 – 2011**<br><br>Head of Finance and Procurement – Menonite Development Associate Tanzania<br><br>**2007 – 2008**<br><br>Regional Financial Controller – International Union for Conservation of Nature (IUCN)<br><br>**2005 – 2007**<br><br>Head of Finance – Action Aid Tanzania |

**DAMAS DAMIAN MUGASHE**



CRDB
BANK
Tunakusikiliza

Tunasonga
mbele